

*Utenzi ujao wa beti nne umeandikwa na Mwamed J.W. Semboja, “Kighono Mbeungwa”
likizungumzia Mke wa Pili*

MKE WA PILI

- | | |
|--|--|
| <p>1. Usiniambaie papale, mama na baba aliko.
na watu waje tele, kujua shauri lako.
Leo ni pweke tukele, na washauri hawako.
Hili langu ndilo lako, au una jinginele.</p> <p>2. Wanizidia machungu, kuongea sikitiko.
kutoshusha moyo wangu, kwa hali ya pujuliko.
Ni ipi hatia yangu, Nilikoikosa kwako.
Hili langu ndilo lako, au una jinginele.</p> | <p>3. Unambiapo si tua, muungwana mwenye mbeko.
Mtukufu wa muruwa, mwelewa na matamko.
sifanye isiyokuwa, nitoa langu sumbuko.
Hili langu ndilo lako, au una jinginele.</p> <p>4. Kwamba huna haja nami, usinionye vituko
nijinyamile sisemi, kwako wewe sina suko
Satui wangu ulimi, sinyemi sina kicheko.
Hili langu ndilo lako, au una jinginele.</p> |
|--|--|

*Mwamed J. W. Semboja (Kighono Mbeungwa)
Oslo, Norway
August, 2002*